

haki kwa wanawake

Women's Initiatives for Gender Justice



Anna Paulownastraat 103, 2518 BC The Hague, the Netherlands Tel: +31 (0)70 365 2042
Fax: +31 (0)70 392 5270 info@iccwomen.org www.iccwomen.org

KURTI ISIYO NA MPAKA, WATESWA, USAIDIZI NA UKINGO

Makubaliano inayounganisha inchi mbalimbali za ulimwengu iliyoshimika kurti (statut de ROME) inaonyesha wazi ya kama victime na mashahidi wao wana haki ya ukingo na kuhudumiwa. Kurti inalazimishwa kukinga wale wote wanaweza kuhatarishwa kwa ajili ya usaidi ama wale wanaostaki mbele ya kurti. Kuwatunza kimafikiri na hata namna yeyote ya usaidizi wanaohitaji. Kurti inapashwa kuhakikisha ukingo wa kimafikiri na kimwili, umutu na heshima ya maisha yao ya upekee.

Ukingo

Kurti sherti iendeleshe utafuti wake pasipo kuhatarisha mtu. Mafasirio ama vihakikisho (preuves) haviwezi kuoneshwa. Sherti vifichwe na kufanya namna yote visihatarishe wale nawaoshiriki kwa kazi ya kurti. Ikiwa mtu fulani amepatwa na shida ama anakuba katika hatari ya kifo kwa sababu aliungana na kurti katika kazi ya utafuti ama maelezo, ni lazima kurti imutafutie ukingo kwa namna ya upekee. Inawezekana iwe hata uhamisho pahali pa utulivu.

Wakati wa masambo, mteswa na mashahidi wao wanaweza kuomba majina yao ifichwe, sura na sauti yao ibadirishwe wanapoleta maelezo yao mbele ya kurti, ama wanaweza kuzungumuza kwa siri. Kurti sherti iwachunge kwa namna ya upekee wale wanaovunjika moyo wakati wanaposhahidia. Kwa mfano watoto, wazee, na wanawake waliobakwa. Wahamuji wanamapasho ya kufanya namna yote victime na mashahidi wake wasivunjike moyo ama kuogopeshwa hasa wale wenyi kubakwa.

Kurti inapashwa kuwapa mashauri, matunzo ya afya ikiwa wanamahitaji hiyo na usaidizi kazalika wakati wanapo ngojea kuleta mafasirio na wakati wa masambo. Kwa namna hii kurti inapashwa kushurulikia kwa namna ya upekee mahitaji ya wanawake, watoto, wazee, vilema na wale waliyobakwa.

Mbele ya kuanza safari yeyote ikiwa mtu ameitwa kusamba mbele ya kurti (Hollande) sherti mganga amtazame kwa kuhakikisha afya yake kimwili na kimafikiri. Kurti inapashwa kusindikiza mteswa na mashahidi wakati wote wasafari tangu wameanza safari kutoka kwa inchi yao hadi watakapo fika pahali kurti ilipo. Iwe kwa kwenda ama kwa kurudi.

November 2004